## HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA CHA TAREHE 07.02.2022 KATIKA UKIIMBI WA MANISPAA WA LEWIS KALINJUNA.

**WAJUMBE**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Elias R. Masumbuka | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe Esther Makune | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Juma Nkwabi | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hassan Mwendapole | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Sheila Mshandete | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mariam Nyangaka | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Gulamhafeez Mukadam | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Getruda Gisema | Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa (Katibu) |

**WASIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Patrobas Katambi (MB) | Mjumbe | - Kwa taarifa |

**MAHUDHUR1O**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | January Mlsana | Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 2. | Salome Komba | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 3. | Salu Ndongo | Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipangomiji |
| 4. | Erick Rwamtoga | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika |
| 5. | Neema Mkanga | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi. |
| 6. | Charles Kafutila | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi. |
| 7. | Nickson Itogolo | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara. |
| 8. | Mwl. Lucas Mzungu | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 9. | Dr Elisha Robert | Mkuu wa Idara ya Afya |
| 10. | Lucy Sewe | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 11. | James Mduma | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Nyuki. |
| 12. | Sifa Amon | Kwa niaba ya Mratibu wa TASAF. |
| 13. | Eng Stephen Manyangu | Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 14. | Naely Elias | Afisa Biashara |
| 15. | Saimon Shoo | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi |
| 16. | Rose Matunda | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Sheria. |
| 17. | Marwa Magere | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi. Kaimu Mkuu |
| 18. | Lenard Chepe | wa Kitengo cha TEHAMA |
| 19. | Fidelis Kabuje | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji. |

**SEKRETARIETI**

| | |
|---|---|
| Marcelina Bwathondi | Mwandishi wa Vikao (CC) |

**Agenda za kikao zitakuwa kama ifuatavyo;-**

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala cha tarehe 17.12.2021
4. Yatokanayo na kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala cha tarehe 17.12.2021
5. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Oktoba hadi Desemba,2021.
6. Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Oktoba hadi Desemba,2021.
7. Taarifa ya utendaji kazi Kisekta ya Oktoba hadi Desemba,2021.
8. Taarifa ya mapato na matumizi ya vituo vya Afya ya Oktoba hadi Desemba,2021.
9. Taarifa ya utekelezaji wa CHF iliyoboreshwa ya Oktoba hadi Desemba,2021.
10. Taarifa ya ununuzi wa eneo (Ardhi) litakalotumika kwa ajili ya kuwezesha shughuli za uwekezaji wa miradi ya kilimo cha bustani kwa vikundi vinavyopatiwa 10% ya mapato ya ndani.
11. Mapendekezo ya kununua mashine na vifaa vingine ili kuvipatia vikundi vilivyoomba mikopo 10%.
12. Taarifa ya ombi la kuhamisha fedha za ununuzi wa dawa kutoka kwenye vituo vyenye bakaa kubwa kwenda vituo vyenye madeni akaunti zilizopo MSD
13. Mashauri ya kinidhamu
14. Taarifa ya mapokezi ya fedha za maendeleo kiasi cha TSh 3,150,825,000.00
15. Kufunga kikao

**MUHT.F/A.06/2021/2022 AGO 01: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 6:30 mchana kwa kuwakaribisha Wajumbe kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na utawala. Aliwaeleza wajumbe kujadili agenda kwa ufasaha na kuzingatia muda.

**MUHT.F/A.06/2021/2022 AGD 02: KUTHIBITISHA AGENDA**

Wajumbe walithibitisha agenda 15 za kikao ili ziweze kujadiliwa.

**MUHT.F/A.062021/2022 AGD 03: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA WA TAREHE 17.12.2021.**

Wajumbe walipitia muhtasari ukurasa kwa ukurasa na kufanya marekebisho ya kiuandishi na kiuchapaji kisha ulithibitishwa kwa kusainiwa na kuwa kumbukumbu halali ya vikao vya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

**MUHT.F/A.06/2021/2022 AGD 06: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA OKTOBA HADI DESEMBA, 2021.**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba ,2021 kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ilitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani, fedha za Serikali kuu pamoja na fedha za Wafadhili. Kwa kipindi hiki Manispaa ya Shinyanga iliendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Shughuli hizi zilitekelezwa katika ngazi ya Idara na Kata kulingana na mpango na bajeti ya Halmashauri. Pia kwa kuzingatia majukumu yaliyoainishwa katika Sera, Sheria na miongozo mbalimbali kwa lengo la kuboresha maisha ya wakazi wa Manispaa.Miradi iliyotekelezwa kwa robo hii ilitumia kiasi cha TSh 3,081,192,294 salio ishia TSh 1,953,368,621

Wajumbe waliipokea taarifa wakaijadili na kuipongeza Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga kwa kupeleka fedha nyingi za miradi kiasi cha TSh3,081,192,294 ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Aidha, kwa kipindi hicho orodha ya miradi ya UVIKO iliyotekelezwa kwa kila kituo ilikuwa kama ifuatavyo: -

| | JINA LA MRADI | JINA LA KITUO/SHULE | IDADI | MAKISIO | KIASI POKELEWA | KIASI TUMIKA S/KUU | ASILIMIA MATUMIZI | HALI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | |
| 1 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu | Busulwa | 2 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 2 | ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Chamaguha | Chamaguha | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 3 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Ibinzamata | Ibinzamata | 2 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 4 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Kizumbi | Kizumbi | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 5 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Kolandoto | Kolandoto | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 6 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Masekelo | Masekelo | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 7 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Mazinge ifikapo Juni 2021 | Mazinge | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 8 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa Sekondari ya Mwamalili | Mwamalili | 1 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 9 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Mwangulumbi | Mwangulumbi | 3 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 10 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Mwasele | Mwasele | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 11 | Ujenzi wa Chumba 1 cha darasa Sekondari ya Mwawaza | Mwawaza | 1 | 20,000,000 | 20,000,000 | 20,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 12 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Ndala | Ndala | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 13 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Ngokolo | Ngokolo | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |

| | JINA LA MRADI | JINA LA KITUO/SHULE | IDADI | MAKISIO | KIASI POKELEWA | KIASI TUMIKA S/KUU | ASILIMIA MATUMIZI | HALI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 14 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Old Shinyanga | Old Shinyanga | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 15 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Town | Town | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 16 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Uhuru | Uhuru | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 17 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Sekondari ya Uzogore | Uzogore | 2 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| | | | **49** | **700,000,000** | **700,000,000** | **700,000,000** | **100** | |
| | | | | | | | | |
| | | | | | | | | |
| 1 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Shule Shikizi ya Mwamashele | Mwamashele | 4 | 60,000,000 | 60,000,000 | 60,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 2 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Shule Shikizi ya Itogwang'olo | Itogwang'olo | 3 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 3 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Shule Shikizi ya Mwamagulya | Mwamagulya | 3 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| 4 | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu Shule Shikizi ya Zaire | Zaire | 3 | 40,000,000 | 40,000,000 | 40,000,000 | 100 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| | | | **14** | **180,000,000** | **180,000,000** | **180,000,000** | **100** | |
| | | | **63** | **880,000,000** | **880,000,000** | **880,000,000** | 100 | |

**MUHT.F/A.06/2021/2022 AGD 14: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MAENDELEO KIASI CHATSH 3,150,825,000.00**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa kuwa Halmashauri ilipokea kiasi tajwa hapo juu kutoka serikali kuu kwa ajili ya kukamilisha majenzi ya elimu sekondari na kutekeleza shughuli mbalimbali za macndelco kwa mchanganuo ufuatao: Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa katika Sekondari ya Ibinzamata TSh 25,000,000, Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa katika Sekondari ya Mwasclc TSh 12,500,000, Ukamilishaji wa vyumba 3 vya madarasa katika Sekondari ya Ngokolo TSh 20,000,000, Ukamilishaji wa vyumba 2 vya madarasa katika Sekondari ya Mazinge TSh 25,000,000, Ukamilishaji wa chumba 1 cha maabara katika Sekondari ya Chamaguha TSh 30,000,000

Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Matumizi ya fedha yanasubiri maamuzi ya kikao cha mfuko wa jimbo TSh 38,325,000.00

Fedha za SEQUEP-T Kwa ajili ya Ujenzi wa Shule maalum ya Wasichana Butengwa Kata ya Ndembezi. Kuanzisha Shule mpya maalum ya Wasichana eneo la Butengwa Kata ya Ndembezi TSh 3,000,000,000

Wajumbe walipokea taarifa na kuipitisha wakisisitiza kuwa ujenzi uanze kwa haraka na kuzingatia ubora.

**MUHT.F/A.06/2021/ 2022 AGD 15: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 9:40 jioni kwa kuwashukuru wajumbe na wataalamu kwa ushiriki wao na ushirikiano walionesha kwa Naibu Meya kwa kipindi ambacho alichokuwa anasimamia Halmashauri, alisisitiza kusisitisha ushirikiano huo uendelee kwake (Mstahiki Meya) ili kudumisha amani katika Halmashauri.

UMETHIBITISHWA

Jomaary M Satura
**KATIBU**

NKURUGENZI YA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
SHINYANGA

Mhe Elias R Masumbuko
**MWENYEKITI**

TAREHE 16/2/2022